JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

# Mwongozo wa Huduma za Utafiti

Disemba, 2018

# IKISIRI

Huduma ya Utafiti ni moja ya nguzo muhimu sana kwa Bunge letu kuwa bora zaidi. Hii ni huduma muhimu kwa kuwa ni moja ya chanzo mbadala kinachotoa taarifa zisizoegemea upande wowote wa kisisasa, hivyo, Wabunge wanaweza kupata taarifa au majibu ya maswali yao bila ya kuwa na wasiwasi.

Utafiti wa kibunge ni tofauti na tafiti zilizozoeleka, kama vile tafiti za kitaaluma ***(academic research)***, kwa kuwa utafiti huu ni wa kutafuta taarifa au data ambazo zimeshafanyiwa utafiti na taasisi za serikali au vituo vingine vya kitafiti vya ndani na nje ya nchi.

Kwa kuzingatia umuhimu wa utafiti, mwongozo huu umetayarishwa ili kuwasaidia na kuwaongoza Wabunge jinsi ya kupata huduma zitolewazo na Idara ya Maktaba na Utafiti katika Sehemu ya Utafiti, na pia utawasaidia wandaaji wa tafiti za kibunge katika kutoa huduma kwa watumiaji wa tafiti hizi. Aidha, mwongozo huu umejumuisha kiambatisho cha vyanzo vya taarifa mbalimbali ambazo hutumika katika utafiti kutoka tovuti mbalimbali zinazohusika na utafiti, takwimu na wachapishaji katika majarida na vitabu.

# YALIYOMO


| | |
|---|---|
| **IKISIRI** | **i** |
| **SEHEMU YA KWANZA** | **1** |
| 1.0 UTANGULIZI | 1 |
| 1.1 UMUHIMU WA HUDUMA ZA UTAFITI KATIKA BUNGE | 2 |
| 1.2 MAJUKUMU YA SEHEMU YA UTAFITI | 3 |
| **SEHEMU YA PILI** | **5** |
| 2.1 CHAMBUZI ZINAZOFANYWA NA SEHEMU YA UTAFITI | 5 |
| 2.2 MAWANDA YA HUDUMA ZA UTAFITI | 6 |
| **SEHEMU YA TATU** | **7** |
| 3.1 JINSI YA KUPATA HUDUMA ZA UTAFITI | 7 |
| 3.2 UTARATIBU WA KUFANYA UTAFITI WA KIBUNGE | 8 |
| 3.4 NYENZO MUHIMU KWA AJILI YA UTAFITI | 9 |
| 3.4 MUUNDO WA TAARIFA ZA UTAFITI | 10 |
| 3.5MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA UTOAJI WA HUDUMA ZA UTAFITI | 11 |
| 3.4 MUUNDO WA TAARIFA ZA UTAFITI | 14 |
| 3.6 HITIMISHO | 12 |
| **VIAMBATISHO** | **13** |
| 1.FOMU | 13 |
| 2. ORODHA YA VYANZO VYA TAARIFA MTANDAONI (TOVUTI) | 14 |

# SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Utafiti ni uchunguzi unaotumia mbinu za kisayansi katika kupata taarifa mahsusi juu ya jambo fulani ili kujua ukweli juu ya jambo hilo. Vile vile, utafiti ni uchunguzi wa siri wenye mpangilio unaofanywa ili kuongeza ujuzi na uelewa kuhusu jambo au tukio lolote liwalo. Aghalabu hutumika katika kuhakiki ukweli wa mambo na desturi.

Ili tafiti inayofanyika iwe na umuhimu ni lazima iwe na pande mbili, yaani upande wa waandaaji wa tafiti hizo (producers) na watumiaji wa taarifa hizo (consumers). Katika kufanya tafiti za kibunge Idara inayohusika na masuala ya tafiti ndio waandaaji na watumiaji ni Wabunge na Maafisa wa Bunge. Wabunge wanahitaji kupata taarifa sahihi zilizofanyiwa utafiti wa kutosha tena kwa wakati muafaka ili kuwasaidia katika kazi zao za kutunga sheria, uwakilishi na kuisimamia serikali.

Hata hivyo, ni vigumu kwa Mbunge kujua na kuchambua masuala yote yahusuyo nchi yake na kwa nyanja zote za kiuchumi, kisiasa, jamii na kiutamaduni bila ya msaada wa mtafiti.  Hivyo huduma za utafiti zinazotolewa na Sehemu ya Utafiti ya Idara ya Maktaba na Utafiti, zinalenga kumsaidia Mbunge kuchambua masuala hayo na kumpa Mbunge taarifa hizo kwa wakati muafaka na kumwezesha kutoa mawazo na michango yake anapotekeleza kazi zake za kibunge.

## 1.1 UMUHIMU WA HUDUMA ZA UTAFITI KATIKA BUNGE

Sehemu ya Utafiti ipo kwa ajili ya kuwawezesha Wabunge na Watumishi kupata taarifa na takwimu muhimu za kuwasaidia kutekeleza majukumu yao vema. Hivyo, huduma za utafiti katika Bunge ni muhimu kwa kuwa zinawawezesha watumiaji wa huduma hii:-

i. Kupata taarifa sahihi na za uhakika zilizofanyiwa utafiti wa kina kuhusu masuala mbalimbali yatakayowasaidia katika kazi zao za kibunge, bila kuegemea itikadi za kisiasa, dini, umri wala jinsia.

ii. Huduma za utafiti ni chanzo mbadala cha kupata taarifa zitakazowawezesha Wabunge kufanya maamuzi sahihi.

iii. Kurahisisha kazi za Wabunge za uchambuzi wa sera, miswada na mipango ya Serikali pamoja na masuala mbalimbali ya kibunge.

iv. Kuwasaidia Wabunge hasa wasio na muda au uelewa wa kutosha kuhusu jambo linalojadiliwa katika uchambuzi wa masuala mbalimbali ya kibunge.

v. Kusaidia kupata taarifa kwa ufupi na kwa wakati, uchambuzi makini kuhusu mitazamo tofauti kwenye masuala yanayohusu Sera za Umma na miswada inayopendekezwa.

vi. Kuwasaidia viongozi wa Bunge na Wabunge kupata taarifa sahihi kuhusu vyama au taasisi za Kibunge za Kimataifa ambazo Bunge ni mwanachama ili kuwawezesha kufanya maamuzi sahihi yanayohusu taasisi hizo kwa manufaa ya Bunge letu.

vii. Kupunguza gharama kwa Ofisi ya Bunge kuajiri

wataalamu/washauri ambao hutoza gharama kubwa kwa kufanya tafiti za kibunge.

viii. Kutofautisha tafiti za kitaaluma ambazo mara nyingi ni kubwa na za kinadharia zaidi, hivyo kutumia dondoo za tafiti hizo katika kuandaa tafiti za kibunge.

ix. Kutoa uchambuzi usiofungamana na upande wowote ule wa kisiasa na kuwasilisha taarifa za uchambuzi huo katika misingi iliyozingatia taaluma na weledi zaidi.

## 1.2 MAJUKUMU YA SEHEMU YA UTAFITI

Majukumu ya Wabunge ni kutunga sheria, kuwakilisha wananchi na kuisimamia Serikali inayowajibika kuwawezesha wananchi kupata huduma za kijamii. Kuwajibika kwa Serikali kunategemea uimara wa Bunge, kwa maana ya uimara na weledi wa Wabunge wake. Hivyo ili Mbunge awe imara na mweledi, anahitaji kupatiwa taarifa sahihi na kwa wakati. Utafiti unaofanywa na Idara ya Maktaba na Utafiti ni muhimu katika kuhudumia Bunge, hasa Kamati za Bunge. Hivyo, Sehemu ya Utafiti ina majukumu yafuatayo:-

i. Kufanya utafiti kulingana na ombi la Mbunge au Kamati ya Bunge ***(information request).***

ii. Kuandaa taarifa fupi kuhusu jambo fulani au sera ***(issue/policy briefs).***

iii. Kuandaa mada mbalimbali ambazo Mbunge au Viongozi wa Bunge wanahitaji kuwasilisha katika semina au warsha za kitaifa au kimataifa ***(background papers and speeches)*** au kupewa dondoo muhimu kuhusu jambo fulani ***(infopack/talking notes).***

iv. Kuchambua muswada kwa kushirikiana na Idara ya Kamati za Bunge na Ofisi ya Mwanasheria wa Bunge.

v. Kuandika taarifa za awali kuhusu jambo au eneo fulani ambalo Wabunge watatembelea ***(Outgoing delegation).***

vi. Kuandika taarifa za awali kuhusu jambo au eneo fulani linalowahusu wageni kutoka sehemu mbalimbali duniani ***(Incoming delegation).***

vii Kuandika taarifa za awali kuhusu jambo au eneo fulani ambalo Wabunge watatembelea ***(Incoming delegation).***

vi. Kutoa elimu kwa wabunge kuhusu namna ya kupata taarifa sahihi kupitia mitandao ya kompyuta (internet based research ***(internet based research).).***

vii. Kuandaa taarifa ambayo Idara inaona inaweza kuhitajika wakati wowote iwe katika Kamati au Bunge ***(anticipated research).***

# SEHEMU YA PILI

Sehemu ya pili ya mwongozo huu inalenga kutoa maelezo juu ya aina za chambuzi na mawanda ya utoaji wa huduma za utafiti.

## 2.1 CHAMBUZI ZINAZOFANYWA NA SEHEMU YA UTAFITI

Sehemu ya utafiti hufanya chambuzi mbalimbali zikiwemo chambuzi za taarifa za utekelezaji wa shughuli za Wizara; Sera mipango na miswada; Sheria na utekelezaji wake; Bajeti na Uchumi n.k. Katika kufanya chambuzi hizo watafiti huzingatia yafuatayo:-

i. **Uchambuzi wa jumla na maombi ya mtu mmoja mmoja *(general and customized analysis).***

Uchambuzi wa jumla hujumuisha kazi zote kuhusu mada mbalimbali zinazofanywa na Sehemu ya Utafiti wakati wote na kutumika pale zinapohitajika. Kwa upande mwingine, maombi ya mtu mmoja mmoja ni ule ambao hutokana na maombi ya Mbunge mmoja mmoja, Kamati ya Bunge, Tume ya Bunge, hali kadhalika vyama vya kibunge kama vile TWPG, TAPAC, APNAC n.k.

ii. **Uchambuzi wa kila siku na wa mahitaji maalum**

Mtafiti hufanya kazi za uchambuzi wa taarifa mbalimbali kila siku na uchambuzi wa mahitaji maalum ili taarifa zake zitumike pale zinapohitajika. Inapotokea kuna hitaji maalum la Mbunge, basi mtafiti atashughulikia hitaji hilo kwa kuzingatia uharaka wa jambo husika. Kwa kawaida, Mbunge huhitaji kufanyiwa chambuzi kulingana na hitaji lake maalum, lakini pia huhitaji kufahamu juu ya masuala mbalimbali yanayojitokeza kila siku ***(topical issues).***

iii. **Uchambuzi kati ya Taarifa za siri na wazi *(confidentiality and transparency)***

Utafiti wa kibunge unafanywa katika taasisi ya kisiasa, hivyo katika kufanya uchambuzi, watafiti wote wanatakiwa kuhakikisha taarifa za kitafiti zinahifadhiwa katika usiri na hazitolewi mahali pengine bila ruhusa ya mwombaji wa taarifa hizo. Kwa kufanya hivyo wabunge wataiona sehemu ya utafiti kuwa ni salama kwa kupata taarifa wanazozihitaji. Aidha, pale taarifa hizo zinapohitajika kwa maslahi ya Bunge zima, watafiti hutakiwa kuwasiliana na Mbunge husika aliyeleta ombi la kufanyiwa tafiti ili kupata ridhaa ya kutumika na Wabunge wengine.

## 2.2 MAWANDA YA HUDUMA ZA UTAFITI

Pamoja na uwanja mpana wa huduma zitolewazo na Sehemu ya Utafiti, mambo yafuatayo yanapaswa kuzingatiwa:

i. Huduma za utafiti zitatolewa kwa shughuli za kibunge tu. Hazitatolewa kwa kazi binafsi za Mbunge.

ii. Kipaumbele cha huduma za utafiti kitatolewa kwa kuzingatia umuhimu na uharaka wa jambo husika.

iii. Mtafiti hatatoa mwongozo au maoni binafsi wa jambo linalojadiliwa, bali atatoa dondoo kuhusu jambo hilo, kama lilivyo kwa wakati husika.

iv. Mbunge haruhusiwi kuomba taarifa binafsi za Mbunge mwingine au mtumishi wa Bunge, imani za kidini au taarifa za kiintelejensia kuhusu Bunge au Taifa lingine.

# SEHEMU YA TATU

Sehemu ya hii ya mwongozo inalenga kutoa ufafanuzi wa jinsi ya kupata huduma za Utafiti, nyenzo muhimu kwa ajili ya kufanya utafiti, utaratibu wa kufanya utafiti, muundo wa taarifa za tafiti za kibunge na mambo ya kuzingatia katika utoaji wa huduma za utafiti wa kibunge.

## 3.1 JINSI YA KUPATA HUDUMA ZA UTAFITI

i. Huduma ya utafiti itatolewa kulingana na:-

a) Ombi la Mbunge mmoja mmoja;
b) Ombi la kundi la Wabunge kama Bunge kwa ujumla; Kamati za Bunge, Tume ya Bunge,Vyama vya Kibunge;
c) Ombi kutoka Ofisi ya Spika au Naibu Spika;
d) Ombi kutoka Ofisi ya Katibu wa Bunge.

ii. Fomu ya Maombi ya Utafiti:

Mbunge anayehitaji kufanyiwa utafiti atajaza fomu maalumu iliyoandaliwa na sehemu ya Utafiti. Aidha kwa Kamati za Bunge na vyama vya Kibunge, Katibu wa Kamati/dawati atajaza fomu hiyo kwa niaba ya Kamati/ dawati lake. Fomu hiyo itakuwa na vipengele vifuatavyo:-

a) Jina la muombaji;
b) Cheo/ Wadhifa;
c) Ofisi au Jimbo la mwombaji;
d) Aina ya tafiti anayohitaji;
e) Lengo la tafiti hiyo;
f) Tarehe ya maombi ya utafiti;
g) Tarehe ya kuhitajika kazi hiyo;
h) Sahihi ya mwombaji.

iii. Pia, Mbunge kutokana na uharaka wa jambo alilonalo anaweza kwenda mwenyewe kwa Katibu wa Bunge au Mkurugenzi wa Idara ya Maktaba na Utafiti ili kuomba taarifa, nyaraka au data anazohitaji. Kama utafiti unaoombwa na Mbunge utakuwa unahitaji taarifa za siri au Usalama wa Taifa, Mbunge atashauriwa kuandika barua kwa Katibu wa Bunge kuomba kibali cha kupata taarifa hizo.

## 3.2 UTARATIBU WA KUFANYA UTAFITI WA KIBUNGE

Huduma za utafiti Bungeni zinalenga katika kutoa tafiti na taarifa ***(information Research)*** juu ya mambo mbalimbali yaliyo katika nyanja zote za kiuchumi, kisiasa, kijamii, na kiutamaduni. Aidha, kama utafiti utahitaji taarifa kutoka nje ya kituo ***(field work),*** kazi hizo pia zitakuwa katika mfumo huu huu wa kutumia vyanzo vingine vya tafiti na taarifa. Hivyo basi, katika kuhakikisha jambo hili linafanyika ipasavyo, huduma ya utafiti itatakiwa kufuata taratibu zifuatazo:-

i. Uelewa au utambuzi wa swali au tatizo ***(problem identification)***

ii. Utambuzi/ uainishaji wa namna ya kutatua tatizo kulingana na;
   a) Aina ya tafiti inayotakiwa;
   b) Aina ya chambuzi unaotakiwa;
   c) Aina na kiwango cha takwimu zinazotakiwa;
   d) Aina ya taarifa zinazotakiwa.

iii. Kukusanya takwimu na taarifa zinazotakiwa.

iv. Kufanya uchambuzi wa takwimu hizo.

v. Kutoa matokeo au ripoti ya utafiti.

## 3.3 NYENZO NA MASUALA MUHIMU KWA AJILI YA KUFANYA TAFITI

i. Maktaba – maktaba ni chanzo cha maarifa ambapo mtafiti anatakiwa kukitumia kupata taarifa za awali ***(literature review)*** zitakazomsadia kuandaa tafiti zake. Katika maktaba, mtafiti atapata taarifa kupitia vitabu, magazeti, hotuba, sheria, taarifa za kihistoria, Hansard, taarifa za mtandao, taarifa za tafiti zilizokwishafanyika n.k.

ii. Mtandao wa Intaneti ***(network)*** kwa ajili ya kutafuta taarifa za kidijitali.

iii. Kompyuta kwa ajili ya kutafuta data, kukusanya data na kuandika kazi za Utafiti.

iv. Karatasi, kalamu, mashine ya kudurufu karatasi, printa, skana, projekta, kamera na vishikwambe, kwa ajili ya kurahisisha kazi za utafiti.

v. Mafunzo ya mara kwa mara ya utafiti ili kuwajengea uwezo watafiti.

vi. Kushiriki katika mikutano, warsha, semina na makongamano ya kibunge kitaifa na kimataifa ili kupata uelewa na ueledi wa mambo y a kibunge yanayojadiliwa katika mikutano hiyo.

vii. Rasilimali watu ya kutosha ili kusaidia kufanyika kwa kazi nyingi za uchambuzi na kukidhi mahitaji ya Wabunge.

viii. Ushirikiano na wadau na Taasisi nyingine za Kitafiti ili kubadilishana taarifa.

ix. Ujuzi wa kitaalam katika mambo yafuatayo:-

a) Uelewa mkubwa wa mambo ya uchumi, siasa, sheria, elimu n.k;

b) Uelewa wa ombi na namna ya kulitatua kwa namna ya kujua sehemu ambayo taarifa inayohitajika itapatikana;

c) Ujuzi wa kufanya kazi ya Utafiti;

d) Ujuzi wa uandishi wa taarifa na ripoti za Utafiti;

e) Ujuzi wa kusoma na kutafsiri data;

f) Ujuzi wa matumizi ya kompyuta na TEHAMA;

g) Ujuzi wa mawasiliano (communication skills).

## 3.4 MUUNDO WA TAARIFA ZA TAFITI ZA KIBUNGE

Wabunge wana shughuli nyingi wanazotekeleza ukilinganisha na muda mchache walionao. Baadhi yao wanaweza kutenga muda wa kutosha kusoma taarifa ndefu za utafiti, lakini wengine wanakosa muda huo. Kwa hiyo uandishi wa taarifa za utafiti wa kibunge unazingatia muda wa Mbunge kutekeleza majukumu yake mengine na Muundo wa taarifa hizo utategemea aina ya taarifa iliyohitajika.

**A. Taarifa Fupi *(Memo/Briefs)*** zenye kurasa 1 au 2 hutumika pale wakati mbunge anapohitaji taarifa fupi juu ya jambo maalum.

**B. Taarifa ya Kawaida** (kurasa 2 -5). Taarifa hii itakuwa na muundo wenye kuonyesha yafuatayo:

i. Mada/ Somo la Utafiti

ii. Utangulizi

iii. Uchambuzi

iv. Athari kwenye sera

v. Hitimisho (wakati mwingine hii sio lazima iwepo)

**C. Taarifa ya Kina *(in-depth report).*** Taarifa ya namna hii itakuwa na muundo ufuatao:-

i. Mada/Somo la Utafiti
ii. Ufupisho wa ripoti
iii. Utangulizi
iv. Mapitio ya maandiko
v. Muundo na njia za utafiti
vi. Matokeo ya utafiti
vii. Hitimisho
viii. Athari kwenye sera
ix. Rejea
x. Viambatisho

## 3.5 MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA UTOAJI WA HUDUMA ZA UTAFITI WA KIBUNGE

i. Kufanya tathmini ya taarifa zilizoandaliwa mara kwa mara ili kuzihuisha taarifa hizo ziendane na mabadiliko ya kijamii yanayoendelea.

ii. Kujenga mahusiano mazuri ya kikazi kati ya Ofisi ya Bunge na taasisi nyingine za kitafiti za ndani na nje ya nchi.

iii. Kutoa taarifa za kweli (facts) na sio mawazo binafsi *(opinion)*.

iv. Kufanya kazi kwa kuzingatia mawanda ya kazi za tafiti.

v. Kuelewa mahitaji ya kila Mbunge anayetaka kufanyiwa tafiti.

vi. Kufanya kazi bila upendeleo wala ubaguzi wa kidini, itikadi za siasa ukabila n.k.

vii. Kufanya kazi kwa vipaumbele kwa kuzingatia umuhimu wa tafiti kwa wakati huo.

viii. Kutotoa siri za tafiti zilizoombwa bila idhini ya mwombaji.

ix. Kufanya kazi kwa kuzingatia muda.

x. Kufanya kazi kwa kuzingatia gharama na faida za uchambuzi (***cost benefit analysis***).

xi. Kuhakikisha kuwa kila taarifa za kitafiti zinajumuisha rejea (references)

xii. Kufanya kazi kwa kuendana na teknolojia ili kupata taarifa mapema na kwa haraka.

## 3.6 HITIMISHO

Idara ya Utafiti ni muhimu kwa Wabunge na Watumishi katika kuwapatia taarifa, takwimu, tafiti na makabrasha yanayowezesha kufanya kazi kwa ufanisi. Utafiti kwa ajili ya Wabunge ni vizuri ufanywe na watumishi wa Bunge wenye ujuzi na uzoefu ambao watatumia taaluma yao katika kupata taarifa zinazohitajika bila kutegemea taarifa na takwimu kutoka Serikalini na taasisi zake pekee.

Kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu yao, Wabunge wanahitaji kupata taarifa sahihi kutoka vyanzo sahihi na kwa wakati, kulingana na maombi yao. Sehemu hii ya Utafiti, ipo kwa ajili ya kuwawezesha Wabunge na Watumishi kupata taarifa na takwimu muhimu za kuwasaidia kutekeleza majukumu yao vema, kwa kuwa bila utafiti hauna ujasiri wa kuchangia na kutoa maoni katika mijadala mbalimbali sawa na usemi maarufu ***"No research no right to speak"***

# VIAMBATANISHO

## IDARA YA MAKTABA NA UTAFITI FOMU YA MAOMBI YA KUFANYIWA UTAFITI

**Jaza fomu hii na uiwakilishe kwenye Idara ya Maktaba na Utafiti**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **JINA LA MBUNGE/ MTUMISHI** | | | | | |
| | | | | | |
| **TAARIFA ZA MUOMBAJI** | Jimbo/Idara/Ofisi | | | | |
| | Namba za simu | | | | |
| | Barua pepe | | | | |
| **Tarehe unapohitajika utafiti huu** | Tarehe | | | | |
| **Lengo la utafiti** | Kamati ya Bunge | Kikao cha Bunge | Bajeti | Uundaji wa sera | Mengineyo |
| **Tarehe ya kuwasilisha** | | | Sahihi | | |
| **Aina ya utafiiti unaoombwa.** | | | | | |
| **MATUMIZI YA OFISI** | | | | | |
| **MAONI** | | | | | |
| | | | | | |

## BAADHI YA TOVUTI UNAZOWEZA KUPATA TAARIFA MBALIMBALI ZA KITAFITI

www.tamisemi.go.tz - Tovuti hii inahusika na utoaji wa taarifa mbalimbali kuhusu maendeleo ya mikoa na serikali za mitaa.

www.nbs.go.tz - Tovuti hii inahusika na utoaji wa taarifa rasmi za takwimu mbalimbali nchini Tanzania.

www.ega.go.tz - Tovuti hii inahusika na utoaji wa huduma za mtandao kwa ofisi zote za Serikali kwa wakati, uwazi, urahisi na gharama nafuu.

www.opendata.go.tz - "Open Data portal" inatoa data katika muundo unaoweza kutumika kwa mashine na kutumiwa tena na mtu yeyote. Data iliyotolewa hutumika tu kwa data na habari zinazozalishwa au zilizoagizwa na serikali hasa sekta muhimu za Elimu, Maji na Afya.

www.tzonline.org - Tovuti hii inahusika na utoaji wa habari juu ya masuala ya maendeleo nchini Tanzania.

www.esrf.or.tz - Tovuti hii inahusika na taarifa za ukuaji wa uchumi, ajira, maendeleo ya viwanda, utawala na uwajibikaji, , utandawazi, ushirikiano wa wa kikanda, utoaji wa huduma za jamii, mali asili na utunzaji wa mazingira, ubunifu pamoja na utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu.

www.repoa.or.tz - Tovuti hii inahusika na utoaji wa taarifa juu ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

www.tgnp.org - Tovuti hii inahusika masuala ya usawa/ haki za jinsia, na haki ya kijamii

www.wri.org - Tovuti hii inahusika na hali ya hewa, nishati, chakula, misitu, maji na maendeleo ya majiji.

www.cintl.org - Tovuti hii inahusika na masuala ya kupambana na umasikini, usawa wa kijinsia na haki za wanawake.

www.genderlinks.org.za - Tovuti hii inahusika na masuala ya usawa na haki za kijinsia.

www.cmi.no - Tovuti hii inahusika na masuala ya utafiti wa sayasi ya jamii inayoshughulikia maendeleo ya kimataifa.

www.eassi.org - Tovuti hii inahusika na taarifa za tafiti mbalimbali, utetezi wa haki za binadamu, kujenga uwezo kwa wananchi, mawasiliano na mitandao, jinsia, uongozi na taarifa za masoko.

www.cgdev.org - Tovuti hii inahusika Utafiti wa kujitegemea zenye kusaidia ustawi wa kimataifa.

www.jstor.org - Tovuti hii ni maktaba ya kidijitali kwa wasomi, wanafunzi na watafiti..

http://journals.cambridge.org - Tovuti hii ni jukwaa maalum kwa wasomaji na watafiti kupata taarifa nyingi na kwa haraka.

www.ingentaconnect.com - Huu ni mtandao wenye rasilimali nyingi za machapisho ya kitaaluma.

www.oecd.org/about/publishing. - Mtandao wenye mada za kutosha kuhusu kukuza uchumi na kupambana na umasikini.

http://journals.co.za - Mtandao huu utakuwezesha kupata taarifa za historia ya Africa, biashara, Elimu, Kazi, Sheria, Sheria za Juta, , dawa, Afya, Dini, Sayansi ya Jamii na Ubinadamu.

http://doaj.org - Tovuti hii inatoa orodha ya machapisho ya majarida yenye ubora wa hali ya juu na rahisi kupatikana

www.oapen.org - Mtandao huu ni Maktaba ya mtandaoni yenye machapisho ya kitaaluma hasa ya sayansi ya jamii na masomo ya utu.

www.tawla.or.tz - Mtandao huu ni jukwaa la mawakili wanawake la kujadili na kushirikishana uzoefu na changamoto mbalimbali wanazokutana nazo katika kutekeleza majukumu yao.

www.policyforum.tz.org - Huu ni mtandao unaolenga kupaza sauti za raia wa kawaida kushawishi katika utungaji wa sera zenye kulenga katika kupunguza umasikini, kukuza usawa na demokrasia nchini.

www.hakiardhi.org - Huu ni mtandao wenye lengo la kukuza uelewa na kubainisha haki za umiliki wa ardhi zinajulikana kwa raia hasa wanaoishi vijijini.

Umeandaliwa na:-
Ofisi ya Bunge
S. L. P 941
Dodoma